MAHUBIRI N°16: JUU YA EZEKIELI 33:1-9

(*Ilihubiriwa jumapili asubuhi tarehe 27 aprili 2003 pa Locodjro, Abidjan - Côte d'Ivoire / www.matth25v6.org*)

… Siri hii inaambatana na matukio mengi za asili kama za kisiasa. Siizungumzii zaidi ili nisifanye kuwa ya taifa jambo lililo la ulimwengu yote. Nchi nyingi za Afrika zilipata uhuru kwa mwaka 1960. Na uhuru ulizidi hata kufikia mwaka 2000, imepita miaka makumi ine na tunaona hewa mpya ya viongozi wakizungumzia hapo "kuunda upya". Mtu alingojea kuunda upya sawasawa na nia yake lakini namna ingine ilimulazimishwa na tangu 2000 hata leo tunaona karibu uharibifu mtupu wa Afrika kwa kutafuta kuitengeneza upya. Ndivyo hivyo, kanisa lilitaka uamsho lakini sawasawa na tamaa yake. Ijapokuwa inabidi Mungu aamue na kuhukumu kwanza uwongo! Munaona?

Turudi sasa kwa mashairi za muhimu: Waroma 10: 13-14 na 1Kor.9:16. Na mahubiri haya yanaeleza wima nanyi mulio hapa. Jueni kwamba yote tutakayo ifanya hapa duniani, yatakufa hapa na hayatakuja kwa kumbukumbu mbele ya Mungu. Ila tu matendo yanayorudi katika utaratibu ya wokovu ndio yatakayo dumu hata umilele kwa maana lile ndilo kanzu ya karamu kama inavyo andikwa katika Ufu.19:7-8. Ni kwa ile tuliitwa. Kutangaza Injili ambayo ni habari njema ya katikati ya usiku siyo tu ya lazima lakini ni jukumu. Kuweka mafuta, ni kwa kumbukumbu ya yale mambo yote. Kornelio akapokea Roho kama zawabu kwa woga ya Mungu na ya sadaka zake za siku zote. Ikiwa kweli umezaliwa upya, inabidi jambo moja lifanyike ndani mwako unapo kutana na Kweli kama yule mwanamke musamaria kwani ndani kuna uzima, kuchochelewa itakayo jitokeza. Japo, zambi kubwa sana jangwani ni kugundua maji na kuyaficha watu. Tangazeni ujumbe huu ili wale iliyo waahidiwa wapate kuipokea. Hatutafuti kugeuza mapondo kuwa samaki wala punda za mwitu kuwa wana kondoo wa Mungu lakini tunalazimishwa kuwaarifu bila kuacha hata mmoja. Hata kama wanasema kwamba ni "hukumu", muifanye! Musizubaishwe!

Zamani za kale, wakristo wa kwanza walihukumu wachawi. Walio watoto wa Mungu walitubu, walichoma uchawi yao na walikubali Kweli lakini wana wa giza, uzao wa nyoka, walisema: "Mungu anasema tusihukumu…" kisha, tangu karne ya XVI, waprotestanti walihukumu kanisa katolika. Kufwatana na Yoane 10, kondoo walitambua sauti ya kiongozi wao na walitoka ili wapate uzima wa milele lakini wana wa ibilisi, wale wale mapepo wa kale walisema "Mungu anasema tusihukumu…". Siku za leo, ni waprotestanti na wale wa kiinjili ndio wanaotumia maneno yale kama ngao. Munaona? Mapepo hayafe kamwe. Haizuru kile watakacho sema, musizubaishwe! Wanabeba mabiblia kama ngozi, hawajui kitu kuhusu Biblia. Wasikie wala wakatae kusikia, muwahubiri mambo yale! Watakwenda kuzimuni lakini wasikie tu. Katika Mt.7:1, imesemwa: "Usihukumu" lakini alisema nini katika Yoane 7:24? Na wakisema ninyi ni wakali, [halafu] "Kizazi cha nyoka! Nyoka katika majani! Kaburi lenyi kupakwa rangi nyeupe!" ni kusema nini? Je! Mimi ni muhubiri wa kwanza kuleta jina kwa wapinzani wa Kweli? Ni wao wasiyo na haki ya kuhukumu lakini kwetu, Mungu alitupa mamlaka ya kuwahukumu kama inavyoandikwa katika 1Kor.2:15! Siyo wao peke lakini pia malaika waliyo anguka ambao ni roho takatifu yao. Tangu Noa, manabii, Yesu-Kristo na mitume, halafu sijui kama unaweza kuhubiri pasipo kuhukumu! Ni Mungu aliye na haki ya kuhukumu na Mungu alinipa uwezo na mamlaka kwa mwandiko na pia kwenu munaoamini ujumbe huu kuwahukumu wale!

Tusome 2Timoteo 2:17. Munaona? Tunaishi kwa wakati ya ubadirishaji wa vibarua na hekima ya watu ilileta chombo ndogo kwa kupima kartasi za benki. Wamoja wana namna ya kutambua tofauti kati ya kartasi ya kweli na ile ya uwongo. Kwa mfano kwa kutazama au kwa kugusa, ile ndiyo inayoitwa karama za kiroho. Mungu alileta kile chombo cha kupima ambacho ni Biblia kwa kuchunguza maroho, mafundisho,…Namna gani mtu anaweza kukasirikia mwenyi kuchunga hazina kwa sababu chombo kilionyesha kwamba kartasi yake ni ya uwongo? Kama kartasi ni ya kweli halafu ni lazima ikusanye hali zote za kartasi ya kweli. Kukiwa na mustari moja tu inayokosa halafu hiyo ni kartasi ya uwongo. Hakuna la kusema kwamba inakaribiana. Ni ile tunayoifanya kwa maroho takatifu wao. Tunaanza kuona mara kwa mara watu pamoja na vitabu vya William Branham kwani haviwezi tena kuleta uzima. Ni Kweli ya wakati fulani. Na mara kwa mara wanafanya wongofu mwingi. Sababu gani? Ndege wengine kubwa kubwa, wakula-maiti na kunguru wanakusanyika pale, wakishangilia na kuruka ruka, kwa wakati tai wanapokuwa kwa Kelele ya katikati ya usiku. Biblia inasema katika Ufu.16:13-14 kwamba ni roho za vyura. Macho ya chura ni juu ya kichwa chake. Anaona kile Mungu alifanya wakati ulio pita, kile atakacho kifanya kwa wakati ujao lakini hapana kile ambacho iko akikifanya [sasa]: "Musa alisema ! Masiya atakuja ijapokuwa Masiya yuko pale! John Wesley, Lutheri alisema, ndugu Branham alisema…" ni huruma!

Mungu aliwaruhusu ninyi kuona Kweli ili muwe sauti ya ile Kweli! Waroma 10:14 *"namna gani watamwamini yule ambaye hawakusikia akitangazwa?"* Musijali masumbuko ya wakati wa leo ambayo ni uadui juu ya wokovu. Kwa mwisho wa kila nyakati, Roho anasema: *"Kwa yule atakaye shinda nitamupa!…"* kama tulishinda zambi za mwili, mafundisho ya uwongo, tusisahau masumbuko ya wakati hii. Tusome Mt.13:22 na Mt.25:24-30, munaona? Ni kweli mumepokea Neno la uzima basi mutalifanyia nini? Kusudi siku moja mbele ya kiti cha enzi cha Mungu wasiseme: sikujua kamwe kwamba kulikuwa Kweli kama hiyo duniani, kwa sababu ningeikubali! Inabidi tufahamu kwamba Mungu anangojea mengi kwetu. Sikieni hiyo mioyoni. Musisukumwe! Kama mtu anajiwazia kuwa na Roho Mtakatifu na anatupilia mbali mahubiri haya ambayo ninaleta, kwa kumwarifu umwambie kwamba aliyo nayo ni roho ya uchawi, hata kama anasema kwa lugha na kufufua wafu. Usiwaache kabla uwaambie maneno haya. Ninasema vizuri: musiwaache kamwe kabla kuwaambia maneno yale. Wakati ya kutisha imepita. Wanabeba mabiblia kwa bure, ni upinde pasipo mishale. Mukitambua, katika Yeremia 26:7-11, ni manabii na makuhani ambao ni wao kwa kawaida wangepaswa kujua Neno hapo ni wao wanao ona kwamba Nabii Yeremia anastahili kufa ijapo kwa shairi la 16, makutano wana maoni iliyo tofauti na yale ya manabii pamoja na makuhani. Munaona? Ni wale wale. Musisukumwe na reverenti, au nabii. Roho na Neno ni moja. Hawapokei Neno hili kwa sababu hawakuumbwa nalo. Walikuja duniani kama michongoma na miba. Wao siyo sehemu ya Neno ndio maana hawalipokei. Ndege zote si tai na hatuwalazimishe kugeuka tai. Ni mahubiri gani munafikiria manabii wa agano la kale walikuwa wakileta na ambayo iliwalazimisha [kupoteza] maisha yao? Na kama tuna Roho moja [nao] basi tutafanya nini? Munaona? Ninapoona wabatisti, wabranhamisti na wengine wakisema: "Tuna Neno" inanikumbusha karamu ya nondo. Ambacho tai hawezi kula, ni kile ndege kubwa kubwa wengine,

ndege za anga wanaolishwa kwa nyama, na vile vikula-maiti wanaita: "Tuna neno, sisi ni katika maandiko". Rehema kwao! Ni kile wamoabu walifanya pamoja na Balama. Ndio maana niliwaambia ninyi musikwende kule.

Vema sana! Turudi sasa kwa lengo letu; na ningependa nitwae mfano wa mtakatifu Martin de Tours mjumbe wa kanisa la Pergamo. Kwa miaka hishirini, kijana askari, nyuma ya ubatizo, alitiwa kwa pumziko kwa ombi lake [mwenyewe] na hakurudi tena kazini mwake kwa maana alitoka kukutana hapana kanisa lakini mtu mmoja, muhubiri Hilaire wa Potiers. Kwa kifo cha Hilaire, mji wa Tours ukaomba Martin awe kama askofu. Tazama ambacho Roma ilijibu: "hatuwezi kufanya kuwa askofu mtu wa kimo ndogo kama huyu, asiyevaa vizuri, asiye chanua vizuri…" kwa kufupisha kwamba mtu mwembamba kama huyo anaonekana kama asiye stahili vema kwa cheo kubwa kama hiki! [Historia ya Kanisa ya mitume na mashahidi, Daniel Rops, ukurasa 243].

Kweli, Roma inazidi kuona watu kama hao ambao hawakupata mafunzo toka kwake, maadui za hatari. Lakini tayari iliwaka ndani mwake moto ambao hakuna awezaye kuizima. Hakati tamaa. Kwa miguu wala kwa punda, kijiji kwa kijiji, kampeni kwa kampeni, makumi ya kusanyiko zinaanza kuonekana, miujiza inafwatana naye. Baadae kanisa likatambua kwake nafasi sawa na ile ya mitume. Maaskofu walimwita lakini hakukutana nao mpaka alipokufa kwa mwaka 397. Zaidi ya makanisa 4000 kubwa kubwa chini ya uongozi wake, vijiji na miji 485 zinao itwa kwa jina lake. Ni kuelekea kujitoa ya namna hii ndipo inatubidi kufikia. Kwa Roma ambayo ilipaswa kujua Neno, alikuwa mtu asiye stahili ijapo ni malaika wa Mungu. Munaona? Kama nilikuwa katika kusanyiko za miungu, singeliweza kuwa kile nilicho kwani sina cheti! Munaona? Tunapendelea mtu aliye jazwa Roho Mtakatifu badala ya mwalimu wa teolojia. Na niliwapa ninyi angalisho juu ya teolojia hata ikiwa ndogo, ni ile Biblia inataja katika Mt.16:5-12. Lakini tunaona uamsho kuu inayo tokana na tamaa ya siku hizi. Baada ya mifano yote katika Biblia na historia ya Kanisa, haifai kungojea malaika ashuke kwa kuwatuma. Hamuifanyi ni kwa sababu hamutaki kuifanya. Musimjaribu Mungu! "Kama Mungu aliniambia nifanye hivi ningeifanya!" Mungu hakumwambia Martin aache kazi. Watu waliona kwamba Hilaire ni mwenye mafundisho ilio kinyume ya ukatolika, aliweza hata kukimbia mbali na nchi yake kwa kuokoa maisha yake. Na ni mtu kama huyu ndiye akawa mwalimu wa Martin. Munaona? Wakristo wanaweka ndoa, watoto, kazi kwa nafasi ya kwanza, na kazi ya Mungu nyuma. Wanatafuta kujua nini watakuwa hapa duniani kabla ya kufikiria juu ya ufalme wa mbinguni na kama kuingia mbinguni inabidi kuwalazimu kujitoa kama vile mitume na watakatifu wa kale, halafu hii ndio hawapendi. Wanatamani kuipokea kama zawadi ya chrismas (noele). Wanapenda ukristo sawa sawa na mtindo ya ubinadamu! Mimi sioni mambo kwa namna hii. Mazungumzo, mikutano na seminari ni majengo ya ubinadamu. Hata yule asiye na huduma, mwanamume kama mwanamke tangu wakati anapo pokea hii Kweli ambayo wengine hawana, inamubidi kwa wakati wowote, kwa matokeo yoyote na hata kwa kubahatisha kidogo, kuitambulisha kwani ndani mwake kunawaka moto kila wakati. Hata unapo tembea unakuwa ukihubiri moyoni, Kweli ndani mwako ni kama mwanamke aliye na mimba, na kukufanya wewe kuwa chemchemi isiyo kauka vile Yesu alivyo mwambia mwanamke musamaria. Kila mahubiri iliyotumwa na Mungu duniani ilikuwa kama Kweli ya upekee inayo paswa kwenda hata mipaka ya dunia: Lutheri pamoja na kuhesabiwa haki, Kalvini pamoja na kutangulizwa, Wesley pamoja na utakaso, William Branham pamoja na nuru ya jioni. Na kama munatambua, wayahudi wanapo waua manabii na wakati ya huyo nabii inapo pita, wanajenga mnara kwa kumukumbuka na wanamutambua kuwa nabii wa kweli. Vivyo hivyo Lutheri alipokuja, alipiganishwa lakini wakati ilipo pita, watu wote wakatambua kwamba alitumwa na Mungu. Na ilikuwa hivi kuhusu Kalvini, Wesley na sasa ni William Branham.

Kupokea Kweli na kuichunga katika kifungo ni upumbavu kwa hao mabikira wa Mathayo 25 na namna gani Mungu anaweza kumjaza mtu na Roho wake kama siyo kwa kupeleka hii Habari Njema? Katika Matendo 4, mitume na wafwasi waliomba kipimo kubwa cha mafuta ili waangaze wale walio katika giza na ilipewa kwao. Ni upumbavu kukamata Kweli kubwa kama hii na kuiweka kifungoni na kuacha watu wafe. Ndio maana mabikira hao walikosa kunyakuliwa na ikawabidi kupita katika mateso makubwa. Ni ile Mathayo 25:14-30; mfano wa talanta ni baki la mfano wa mabikira kumi. Haihusu makanisa za waprotestanti na wakiinjili, wala misioni na huduma, wala wabranhamisti lakini mabikira kumi na kile watakacho fanyia Kweli waliyo pewa na Mungu. Kwani walitenda kwa uovu walipo chunga Kweli kifungoni, wataokolewa kwa mateso makubwa. Kama alivyo andika Ezekieli 33:1-9, tunashurtishwa kutangaza hii Kweli *"kwa kuarifu mwovu kwa ajili ya njia yake"*. Makanisa zote hizo zinaelekea jehanama na utangoja wakuambie uwaarifu? Biblia inasema: *"mwovu atakufa katika uzalimu wake lakini nitataka damu yake kwa zamu"* lakini ukamwarifu na anabaki katika kanisa lake, *"…na haachi njia yake, atakufa katika uzalimu wake lakini wewe umeokoa nafsi yako"* Munaona? Nyumba yetu, wanao tuzunguuka, kampeni, vijiji, miji na nchi na hayo makanisa wanangojea nani? Kila mmoja wetu atajieleza siku moja mbele ya Mungu. Kama mitume ni baba zetu, tufanye kazi ya mitume. Mfano wa talanta inahusu ambacho kila mmoja alifanyia Kweli aliyo ipokea. Munaona? Ukijiweka kwa kazi, karama zitafwatana na kazi.

Fikiria gari moja na mtu nje akipaza sauti: *"Ninyi mulio katika gari hiyo, juweni kwamba gari hiyo haina vibarua, gurudumu zake zimezeeka, breki yake inaharibika hata dereva wake hana barua yakumuruhusu kuendesha gari!"*. Ile ndio kazi yetu. Munaona? Wenye busara watatafuta kuchunguza inayosemwa kwa ugumu kabla gari haija tikisika bado hata kidogo lakini wapumbavu watamujibu: "Wewe ni polisi? Huna budi ya kusema hivi kwani wewe si polisi!". Munaona? Nafsi hawana bei moja…

Tunapoona Mathayo 13:22, tunafahamu upesi sababu ya hali kama hii. Ni kwa kusudi Roho anatia mkazo ili aliye na masikio kwa kusikia, asikie. Katika ono, kulikua na patwa mwezi (jua) na kiisha… ujumbe unaposhuka, mwanga wake unapashwa kuangaza dunia yote na ni ile mabikira waakili walifahamu na ndio maana walipewa sehemu kubwa ya mafuta. Sababu gani mtu asiyefanya kazi atapewa mafuta ya kutosha? Kwa kufanya nini? Hata katika Agano la Kale au Jipya, ni kwa kufanya jambo fulani ndio maana Mungu analeta Roho au mafuta. Mabikira waakili au mabikira wapumbavu, ni tangu sasa ndipo kutengana iko ikipata nafasi. Munaona? Mabikira wapumbavu wao si nje tu lakini wamekaa hapa pamoja na maandamano ya mafikiri kichwani. Hata mtoto wa Mungu anapo tumika, shughuli yake siyo kile alicho nacho katika hesabu yake ya benki hata leo lakini kile alicho kifanya kwa Mungu ili ashiriki kwa kutangazwa kwa Neno.

Mtakatifu Martin akaomba hiyo pumziko na hakurudi tena kwa nafasi yake ya kazi kwa kutumikia nchi yake. Tangu alipoanza mahubiri katika kampeni, hakukuwa ugonjwa au ulema zilizo shindana na maombi yake. Wafu walifufuliwa…

Munaona mambo haya ? Hakukubali malipo, kama Elisa na Naamani, Kama vile Bwana alivyo agiza. Hatuta kubali mali kutoka mtu kwa sababu Mungu alifanya miujiza maishani mwake kwa njia yetu. Na hatupendi kuonekana tukijipatia mali nyingi tungeliweza kuwa nayo kwa kununua viwanja na kujenga mahekalu nzuri, na zenyi kutandikwa vizuri, pamoja na vitambaa kutandikwa chini ijapo mbali watu wanafariki kwa kukosa Neno. Bidii yetu inapswa kuelekea kwanza Neno. Ni hakika sehemu ya pili ya Neno iliyoshuka kutoka mbinguni juu ya mawingu. Sehemu ya kwanza tayari imekwisha na sasa tuko tukitarajia kumaliza sehemu ya mwisho. Maneno ya kwanza yalikuwa hukumu na yale ya pili yalikuwa ya kuambia Kanisa irekebishe maisha yake. Nilisimama hivi na niliona kwa upande wa mashariki maandiko kwa kifaransa inayoshuka juu ya mawingu. Ile inawasemea wateule na hao wataamini. Walisema: *"Hatukuona Malaika na Mwana Kondoo lakini tunaamini KWA UKAMILIFU…"* Munaona? Kunyakuliwa siyo kwa ajili ya kunguru, vyura na ndege kubwa kubwa za unafiki; wala wale wanao ona haya kwa Injili. Hata ninyi wadada, shuhudieni!
Turudi kwa Ezekieli 33, kama vile baba zetu mitume walipiga baragumu, ndivyo kila mmoja wetu ameitwa kuifanya. Kuwa mkristo, ni kufikia nafsi zinazopotea ijapo ni haki yao kusikia Kweli kwa kuokoa nafsi zao. Kuwa mkristo ni kuwa na uzito na huruma kwa nafsi. Aliye na masikio ya kusikia asikie!

MAWASILIANO: Ndugu Filipo:+ 225-0252-0252 E-mail: kacou.philippe@yahoo.fr
Upate mahubiri katika site ya: www.matth25v6.org